25 Aprili 2019

Kupinga Ufadhili wa Usambazaji:

Mafunzo Yaliyong'amuliwa kwenye Mfano wa Usafirishaji wa Chinpo

Imetayarishwa na Beatrice Müller

Utangulizi

Mnamo 13 Julai 2013, chombo cha usafiri cha *Chong Chon Gang* kilizuiwa ili kikaguli we na maafisa wa Panama. Chombo hicho cha mzigo wa kawaida, kilichokuwa kiko njiani kutoka Kuba hadi Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Korea, kilikamatwa k wa ajili ya kushukiwa kuwa kinabeba dawa za kulevya[1]. Hakuna dawa za kulevya ziliz opatikana kwenye chombo hicho. Lakini, uliofinikwa chini ya begi 200,000 za sukari, mzigo mkubwa sana wa silaha (na nyenzo za silaha) ambao ulikuwa unakiuka maruf uku ya silaha iliyowekewa Korea Kaskazini[2] ulipatikana.[3] Miongoni mwa vifaa vya kije

[1] Eda Erol and Leonard S. Spector, "Chinpo Shipping: Wakala ya Fedha ya Korea Kaskazini nchini Singapoo," *Kituo cha Utafiti wa Kupinga Usambazaji cha James Martin Ripoti ya Kanuni ya* 35 (Disemba 2017): 45, http://www.nonproliferation.org/wp-content/uploads/2017/12/op35-part3.pdf (ilifikiwa mnamo 26 Aprili 2019).

[2] Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, *Azimio la 1718 (2006) Kupinga Usambazaji/Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Korea*, 14 Oktoba 2006, S/RES/1718 (2006).

[3] Jopo la Wataalamu ambalo baadaye lilichunguza tukio hilo, liling'amua kuwa mzigo uliokuwa kwenye *Chong Chon Gang* ulikuwa unakiuka marufuku ya silaha iliyokuwa imewekewa Korea Kaskazini na azimio la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa la 1718 (2006) na azimio la 1874 (2009). Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, Kamati ya Vikw

Rico Carisch www.comcapint.com Loraine Rickard-Martin

rico.carisch@comcapint.com 110 West 94 Street – 2D loraine.rickard-martin@comcapint.com

+1-610-390-9541 New York, NY 10025 +1-917-715-2142

shi, vipuri na ndege kamili za MiG-21 zilipatikana, pamoja na bunduki ndogo, silaha nyepesi, na risasi.[4]

Usafirishaji huo ulirahisishwa kupitia malipo ya ada za usafirishaji yaliyotolewa na ka mpuni ya Singapoo, Chinpo Shipping Company (Private), Ltd (Chinpo). Chinpo iliishi a kufunguliwa mashtaka nchini Singapoo kwa uhusishaji wake kifedha kwenye usafir ishaji huo wa bidhaa.

Kwa ajili Chinpo ilifunguliwa mashtaka kwa kufikisha huduma za fedha kwa shirika l a Korea Kaskazini, kesi hiyo ingekuwa ufunguliaji mashtaka wa kwanza unaohusu uf adhili wa usambazaji. Hata hivyo, kama itakavyozungumziwa, kesi ya Chinpo inaony esha matatizo ya kuzuia na kufungulia mashtaka ya ufadhili wa usambazaji silaha. K uchambua kesi hii kunasaidia kuelewa jinsi ufadhili wa usambazaji ulivyo kihalisi na kunaonyesha umuhimu wa utekelezaji wakina wa vikwazo vya Umoja wa Mataifa ili k uhakikisha uzuiaji wenye ufanisi wa usambazaji wa nyuklia.[5]

azo ya 1718 (Korea Kaskazini), “Ripoti ya Jopo la Wataalamu iliyoanzishwa kwa kutii azimio la 1874 (2009),” 6 Machi 2014, S/2014/147, paragrafu ya 78.

[4] Mzigo uliofichwa ulikuwa na mifumo ya makombora ya ardhi-hadi-anga na vijenzi vyake, ndege mbili za MiG-21 ziliz otenganishwa, injini kadhaa za ndege za MiG-21, risasi na nyenzo zingine zinazohusu silaha. Vingi kati ya vitu vilivyo patikana kwenye meli hiyo vilikuwa havijatumika. S/2014/147, paragrafu za 69,72,74; Hugh Griffiths na Roope Siirtola, “Ufichuzi Kamili: Yaliyomo kwenye Meli ya Usafirishaji Haramu ya Korea Kaskazini Yafichuliwa,” *38 Kaskazini*, 27 Ag osti 2013, https://www.38north.org/2013/08/hgriffiths082713/ (ilifikiwa mnamo 26 Aprili 2019); Erol na Spector, “Chinp o Shipping,” 45-46.

[5] Emil Dall, Tom Keatinge na Andrea Berger, “Kupinga Ufadhili wa Usambazaji: Mwongozo wa Utangulizi kwa Taasisi za Fedha,” *Mwongozo wa Utafiti wa Huduma za Royal United* (Aprili 2017): 10.

Enrico Carisch www.comcapint.com Loraine Rickard-Martin

Simu: (610) 390 9541 110 West 94 Street 2-D Simu: (917) 715 2142

Rico.carisch@comcapint.com New York, NY 10025 loraine.rickard-martin@comcapi nt.com

1. Ufadhili wa kujificha wa usafirishaji bidhaa

Tunaweza kujiuliza jinsi usafirishaji wa mzigo huu mkubwa unaokiuka mfumo mpana wa vikwazo uliweza kufichika usijulikane na maafisa wa serikali. Mbali na kuvificha vifaa vya kijeshi visionekane,[6] Korea Kaskazini pia ilitumia mbinu tata ili kuficha mia mala ya fedha inayohusu usafirishaji wa mzigo huo.[7]

Chong Chon Gang ilikuwa inaendeshwa na kusimamiwa na Kampuni ya Usimamizi ya Ocean Maritime, Ltd (OMM), ambayo ilipanga usafirishaji wa mzigo huo.[8] Ili kuepuka ufuatilizi maalum wa shughuli zake za kila siku, OMM iliunda mtandao wa kampuni na wawakilishi wa Asia Kusini Mashariki.[9] Miongoni mwa kampuni hizi ilikuwa Chinpo yenye makao yake makuu nchini Singapoo. Chinpo iliagizwa na OMM ilipe ada za upitishaji wa *Chong Chon Gang* kwenye Kanali ya Panama.[10] Kama ilivyoagizwa, Chinpo ilituma ada hizi kwa wakala ya usafirishaji nchini Panama kupitia akaunti yake kwenye Benki ya Uchina.[11]

---

[6] Chombo cha mizigo mikavu kilichotumiwa kilibadilishwa ili kiweze kubeba makontena chini ya mzigo mkavu iliyoku wa imebeba. Kulingana na Griffiths na Siirtola, matumizi ya wabebaji mizigo mikubwa yalikuwa kama msingi imara wa usafirishaji wa kujificha wa makombora hadi nchini Korea Kaskazini. Tayari kabla ya uwekaji wa vikwazo, chombo cha Korea Kaskazini kilikamatwa mnamo kikiwa njiani kinaelekea Yemeni. Kama kwenye mfano huu, chombo chenye mzigo kilikuwa kinafaa kubeba mzigo mkavu (simiti) tu, lakini ukaguzi uligundua bidhaa za kijeshi chini ya mzigo uliodhihirishwa. Griffiths na Siirtola, "Ufichuzi Kamili"; S/2014/147, paragrafu ya 125.

[7] Erol na Spector, "Chinpo Shipping," 43.

[8] S/2014/147, paragrafu ya 82; Erol na Spector, "Chinpo Shipping," 45.

[9] Erol na Spector, "Chinpo Shipping," 43.

[10] S/2014/147, paragrafu ya 82, paragrafu ya 179.

[11] Mahakama Kuu ya Singapoo, Chinpo Shipping Co (Pte) Ltd dhidi ya Kiongozi wa Mashtaka, SGHC 108 (2017), par. 19; Erol na Spector, "Chinpo Shipping," 46; Andrea Berger, "Kesi ya Chinpo Shipping Inang'amuka," *Arms Control Wonk*, 15 (Mei 2017), https://www.armscontrolwonk.com/archive/1203164/guest-post-the-chinpo-shipping-case-implodes/ (ilifikiwa mnamo 24 Aprili 2019).

Enrico Carisch www.comcapint.com Loraine Rickard-Martin

Simu: (610) 390 9541 110 West 94 Street 2-D Simu: (917) 715 2142

Rico.carisch@comcapint.com New York, NY 10025 loraine.rickard-martin@comcapint.com

Chinpo hapo awali ilikuwa biashara ndogo ya uwakala wa usafirishaji bidhaa na kam puni ya kufikisha bidhaa melini, iliyokuwa inaendeshwa na Tan Cheng Hoe na famili a yake.[12] Uhusiano wa kibiashara wa Tan na Korea Kaskazini ulianza kwenye miaka y a 1970, pale alipoanza kufikisha huduma za biashara baharini kwa mashirika ya Kore a Kaskazini.[13] Baada ya OMM kuanzishwa kwenye miaka ya 1990, Chinpo ilitoa hudu ma zinazohusu usafirishaji kwa OMM.[14] Karibuni, Chinpo ilianza kufanya shughuli ka ma wakala ya malipo na usafirishaji bidhaa ya OMM huko Singapoo – mbali na hudu ma zinazohusu mizigo.[15] Kwa ajili OMM ilikuwa haiwezi kufungua akaunti za benki nc hini Singapoo, OMM ilianza kuitumia Chinpo kwenye miamala yake ya fedha.[16] Hudu ma za fedha zilizotekelezwa na Chinpo zilikuwa zinajumuisha ukusanyaji wa malipo yaliyokuwa yanadaiwa na OMM, kulipa mishahara ya wafanyakazi wa OMM nchini Si ngapoo, na pia kutuma mlipo kwa wamiliki wa vyombo vya usafiri vya Korea Kaskazi ni, kwa OMM, au kwa mashirika mengine huko ng'ambo kama walivyoagizwa na OM M.[17] Chinpo ilifanya hivyo bila kuulizia lengo la malipo hayo.[18] Mbeni ilitathminiwa k

[12] Erol na Spector, “Chinpo Shipping,” 44.

[13] Berger, “Kesi ya Chinpo Shipping Inang'amuka”.

[14] Erol na Spector, “Chinpo Shipping,” 44.

[15] Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, Kamati ya Vikwazo ya 1718 (Korea Kaskazini), “Ripoti ya Jopo la Wataal amu iliyoanzishwa kwa kutii azimio la 1874 (2009),” 24 Februari 2016, S/2016/157, paragrafu ya 139; S/2014/147, pa ragrafu ya 86; Erol na Spector, “Chinpo Shipping,” 54.

[16] Andrea Berger, “Shukrani kwa Benki: Kupinga Ufadhili wa Usambazaji na Kesi ya Chinpo Shipping,” *38 Kaskazini,* 16 Disemba 2015, https://www.38north.org/2015/12/aberger121615/ (ilifikiwa mnamo 26 Aprili 2019); Jonathan Brew er, “Uchunguzi wa Uainishaji wa Ufadhili wa Usambazaji wa Silaha za Maangamizi Makubwa, Ripoti ya Mwisho,” *Mra di Alpha, King’s College London,* 13 Oktoba 2017, https://projectalpha.eu/final-report-typologies-of-proliferation-financ e/ (ilifikiwa mnamo 26 Aprili 2019): 52.

[17] Erol na Spector, “Chinpo Shipping,” 44, 52.

[18] Ibid., 44.

Enrico Carisch www.comcapint.com Loraine Rickard-Martin

Simu: (610) 390 9541 110 West 94 Street 2-D Simu: (917) 715 2142

Rico.carisch@comcapint.com New York, NY 10025 loraine.rickard-martin@comcapi nt.com

wenye taratibu za mahakama kuwa matendo haya yalijumuisha bishara ya kufikisha malipo bila Chinpo kuwa na leseni halali.[19] Mwishowe, Chinpo iliacha kuashiria majin a ya vyombo vya usafiri kwenye miamala husika ili kuzuia maswali ya ziada kutoka k wa benki za nje.[20]

2. Yaliyotokea mahakamani

Kuhusiana na malipo ya Chinpo kwa niaba ya OMM kwenye tukio la *Chang Chon Gan g,* viongozi wa mashtaka wa Singapoo waliwasilisha mashtaka mawili tofauti dhidi y a Chinpo na mkurugenzi wake mnamo Juni 2014: kwanza, kufanya biashara ya kupo kea malipo bila kuwa na leseni halali; na pili, kuhamisha mali au rasilimali ambazo zi naweza kueleweka kuna zinatumia ili kuchangia kwenye shughuli au miradi inayohu su nyuklia ya Korea Kaskazini.[21] Chinpo ilipatikana na hatia kwa mashtaka yote mawi li na mahakama husika ya wilaya nchini Singapoo mnamo 14 Disemba 2015.[22] Hata h ivyo, mahakama kuu ilikataa shtaka moja baada ya rufaa.

[19] Chinpo pia ilitoa nafasi zake za ofisi kwa balozi ya Korea Kaskazini nchini Singapoo na waajiriwa wa OMM. Balozi i litumia anwani ya posta ya Chinpo, na Chinpo ilirahisisha ajira kwa wafanyakazi wa Korea Kaskazini nchini Singapoo. Erol na Spector, “Chinpo Shipping,” 45; Dall et al. “Kupinga Ufadhili wa Usambazaji,” 13.

[20] Ilidaiwa kuwa mwajiriwa wa Benki ya Uchina aliishauri Chinpo isiashirie majina ya vyombo vya usafiri. Uondoaji wa maelezo unaonekana kuwa unaendeleza utendakazi wa ukiukaji wa OMM. S/2016/157, paragrafu ya 192.

[21] Mahakama Kuu ya Singapoo, Chinpo Shipping Co (Pte) Ltd dhidi Kiongozi wa Mashtaka, SGHC 108, 2017, paragr afu ya 1; S/2016/157, paragrafu ya 137; Berger, “Kesi ya Chinpo Shipping Inang'amuka”.

[22] S/2016/157, paragrafu ya 137; Erol na Spector, “Chinpo Shipping,” 47; Berger, “Kesi ya Chinpo Shipping Inang'am uka”; Brewer, “Utafiti wa Uainishaji” 52.

Enrico Carisch www.comcapint.com Loraine Rickard-Martin

Simu: (610) 390 9541 110 West 94 Street 2-D Simu: (917) 715 2142

Rico.carisch@comcapint.com New York, NY 10025 loraine.rickard-martin@comcapi nt.com

Kuhusiana na shtaka la kwanza, hakimu wa wilaya aliamua kuwa Chinpo ilifanya bis hara ya upokeaji malipo bila leseni halali kwa kuwasilisha jumla ya malipo 605 yanay oenda nje yenye thamani ya milioni $40 baina ya miaka ya 2009 na 2013.[23] Baada ya r ufaa, uamuzi huu uliendelezwa na mahakimu wa Mahakama Kuu ya Singapoo.[24]

Kuhusiana na shtaka la pili, Chinpo ilishtakiwa kuwa ilihamisha rasilimali za fedha a mbazo inaweza kueleweka kuwa zinatumiwa kuchangia kwenye mradi wa nyuklia w a Korea Kaskazini.[25] Kesi hii ilijumuisha ufunguaji mashtaka wa kwanza ujulikanao u naohusu ufadhili wa shughuli zinazohusu usambazaji.[26] Kwa hivyo, kulikuwa na ham u kubwa kwa kesi hii mpaka ilipokataliwa kwenye rufaa.

Msingi wa kisheria wa kufungulia mashtaka kuhusiana na shtaka la pili ulikuwa Kanu ni ya 12 (b) ya ‘Kanuni za Umoja wa Mataifa za 2010’ kama ziitwavyo nchini Korea Kaskazini. Kanuni za Umoja wa Mataifa za 2010 zinafasiri vikwazo vya Baraza la Usala ma la Umoja wa Mataifa vilivyowekewa Korea Kaskazini viwe sheria ya Singapoo.[27] K anuni ya 12 (b) imeandikwa kama ifuatavyo:

[23] S/2016/157, paragrafu ya 191.

[24] Berger, “Kesi ya Chinpo Shipping Inang'amuka”; Erol na Spector, “Chinpo Shipping,” 50.

[25] S/2016/157, paragrafu ya 190.

[26] Erol na Spector, “Chinpo Shipping,” 44.

[27] Ibid., 48.

Enrico Carisch www.comcapint.com Loraine Rickard-Martin

Simu: (610) 390 9541 110 West 94 Street 2-D Simu: (917) 715 2142

Rico.carisch@comcapint.com New York, NY 10025 loraine.rickard-martin@comcapint.com

> Hakuna mtu nchini Singapoo waka hakuna raia wa Singapoo nje ya Singapoo—(a) atakaye toa huduma zozote za fedha; au (b) atakayehamisha mali au rasilimali za fe dha, au mali au rasilimali zingine, *ambazo zinaweza kueleweka kuwa zitatumiwa k uchangia kwenye* shughuli na mradi unaohusu nyuklia, unaohusu makombora ya mbali, au unaohusu silaha zingine za maangamizi makubwa za Jamhuri ya Kidemo krasia ya Watu wa Korea.[28]

Kwa ajili ya muundo wa Kanuni ya 12 (b), ilibidi kiongozi wa mashtaka adai kuwa uh amishaji fedha uliofanywa na Chinpo ulikuwa *unaweza kueleweka kuwa utatumiwa ili kuchangia kwenye* mradi unaohusu nyuklia au mradi unaohusu makombora ya m bali ya Korea Kaskazini. Hata hivyo, chombo hicho kilikuwa kinabeba silaha za *kawa ida*.[29] Mahakama ya wilaya ilidai kuwa silaha na nyenzo husika kwenye meli ya *Chon g Chon Gang,* ingawa zenyewe zilikuwa hazihusu nyuklia, lakini zilikuwa zinaweza ku tumia kulinda mradi wa silaha za nyuklia wa Korea Kaskazini.[30] Pia ilidaiwa kuwa mal ipo ya ada za Kanali ya Panama yalichukuliwa kuwa ni malipo yanayohitajika ili kute keleza usafirishaji.[31] Kwa hivyo, mahakama ilidai kuwa malipo yanaweza kuchukuliw a kuwa yalitumiwa ili kuchangia kwenye mradi wa nyuklia wa Korea Kaskazini, na wa kaamua kuwa Chinpo ina hatia kwa kukiuka Kanuni ya 12 (b).

Mtiririko huu wa fikra haukushawishi Mahakama Kuu. Mahakama Kuu ilikosoa uamu zi wa mahakama ya wilaya kwa misingi kuwa yaliyofuata yalikuwa yanafaa kuchamb

---

[28] [Msisitizo umeongezwa]. Sheria za Singapoo Mtandaoni, "Umoja wa Mataifa (Vikwazo - Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Korea) - Kanuni za 2010," S 570/2010, https://sso.agc.gov.sg/SL/UNA2001-S570-2010/Historical/20101101?DocDate=20171019&ValidDate=20101101 (ilifikiwa mnamo 26 Aprili 2019). Tangu hapo, Kanuni za Umoja wa Mataifa za 2010 zimerekebishwa. Ili kupata maelezo ya ziada, tazama kifungu cha 3.1.

[29] Erol na Spector, "Chinpo Shipping," 48.

[30] Mahakama Kuu ya Singapoo, Chinpo Shipping dhidi ya Kiongozi wa Mashtaka, paragrafu ya 71; Erol na Spector, "Chinpo Shipping," 48.

[31] Mahakama Kuu ya Singapoo, Chinpo Shipping dhidi ya Kiongozi wa Mashtaka, paragrafu ya 27.

Enrico Carisch www.comcapint.com Loraine Rickard-Martin

Simu: (610) 390 9541 110 West 94 Street 2-D Simu: (917) 715 2142

Rico.carisch@comcapint.com New York, NY 10025 loraine.rickard-martin@comcapint.com

uliwa ili kung'amua kama *uhamisho* wenyewe ungeweza kuchangia kwenye mradi w a nyuklia wa Korea Kaskazini, badili ya kuthibitisha uhusiano baina ya silaha za kawa ida na mradi wa nyuklia.[32] Mahakama Kuu haikukataa tu dai kuwa silaha za kawaida zilichangia kwenye mradi wa nyuklia. Kwa msingi wa ufasiri uliobanwa zaidi wa Kanu ni ya 12(b), Mahakama Kuu pia ilibainisha kuwa *uhamishaji fedha* haukuweza kutum iwa kuchangia kwenye mradi wa silaha za nyuklia wa Korea Kaskazini. Kulingana na Mahakama Kuu, Kanuni ya 12(b) inachukulia pekee uhamishaji fedha unaoweza kutu mia kupata mali ambayo yanatoa mchango wa *moja kwa moja* kwenye uundaji wa si laha za nyuklia nchini Korea Kaskazini, kama vile kuwa uhamishaji fedha huo ni wa *k upata* silaha ya nyuklia.[33] Hata utumaji malipo ya gharama za usafirishaji wa silaha y a nyuklia pia unaweza kuwa haujumuishwi kwenye upana wa Kanuni ya 12 (b).[34] Kwa hivyo, ufunguliaji mashtaka ya ufadhili wa usambazaji haukufaulu, ambayo ilidhihiri sha baadhi ya matatizo yanayohusishwa kwenye kufungulia mashtaka kesi kama hiz i.[35]

3. Kupinga ufadhili wa usambazaji: Mafunzo yaliyopatikana

3.1 Utekelezaji usio kamili wa maazimio ya Baraza la Usalama la Umoja wa M ataifa kwenye sheria za taifa

Miongoni mwa matatizo haya, lilikuwa tatizo la utekelezaji usio kamili wa maazimio ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa. Kanuni ya 12 (b) ilikuwa inategemea azim

[32] Ibid., paragrafu ya 56

[33] Ibid., paragrafu ya 61.

[34] Ibid., paragrafu ya 58.

[35] Erol na Spector, “Chinpo Shipping,” 47, 48, 50.

Enrico Carisch www.comcapint.com Loraine Rickard-Martin

Simu: (610) 390 9541 110 West 94 Street 2-D Simu: (917) 715 2142

Rico.carisch@comcapint.com New York, NY 10025 loraine.rickard-martin@comcapint.com

io la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa la 1874 (2009), lakini azimio lilikuwa hali jatekelezwa kikamilifu kwenye sheria za taifa.[36] Paragrafu ya 18 ya azimio la 1874 (20 09) ilitoa mwito kwa nchi wanachama zizuie ufikishaji wa huduma za fedha ambazo zingeweza kuchangia kwenye miradi inayohusu nyuklia, inayohusu makombora ya mbali, au miradi mengine inayohusu silaha za maangamizi makubwa za Korea Kaska zini.[37] Kwa ajili Kanuni ya 12 (b) ilikuwa inategemea paragrafu hii pekee, paragrafu zi ngine muhimu zilipuuzwa. Ambayo ni muhimu zaidi ingekuwa utekelezaji wa paragr afu za 9 na 10 ambazo zilikuwa zinakataza miamala ya fedha inayohusu silaha za ka waida.[38] Kwa hivyo, utekelezaji mpana wa maazimio husika ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa ungewezesha kupigwa marufuku huduma za fedha zinazochangia kwenye uhamishaji wa silaha za kawaida.

Kanuni ya 12 (b) ya Kanuni za Umoja wa Mataifa za 2010 tangu hapo imerekebishwa i li kushughulikia baadhi ya upungufu huu.[39] Marekebisho hayo yalitanguliza kukataza

[36] Ibid., 48.

[37] Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, *Azimio la 1874 (2009) Kupinga Usambazaji/Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Korea*, 12 Juni 2009, S/RES/1874 (2009), paragrafu ya 18; Mahakama Kuu ya Singapoo, Chinpo Shipping dhidi ya Kiongozi wa Mashtaka, paragrafu ya 45.

[38] Berger, “Kesi ya Chinpo Shipping Inang'amuka”; S/RES/1874 (2009), paragrafu ya 9, paragrafu ya 10.

[39] Kanuni za Umoja wa Mataifa za 2010 zimerekebishwa *miongoni mwa zingine* na “Umoja wa Mataifa (Vikwazo – Ja mhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Korea) (Rekebisho) Kanuni za 2017”, S 590/2017, https://sso.agc.gov.sg/SL-Supp/S590-2017/Published/20171019?DocDate=20171019 (ilifikiwa mnamo 26 Aprili 2019).

Kanuni ya 12 (b) kama ilivyorekebishwa na S 590/2017 sasa ina kichwa cha “Katazo dhidi ya ufikishaji wa huduma za fedha na rasilimali zingine zinazochangia kwenye shughuli isiyoruhusiwa” na imeandikwa kama ifuatavyo: “12. (1) Mt u nchini Singapoo au raia wa Singapoo nje ya Singapoo ni lazima, moja kwa moja au kivingine (a) aitoe huduma zoz ote za fedha (zikiwemo kutoa mikopo ya uuzaji nje, udhamini au bima); wala (b) asihamishe mali au rasilimali za fedh a, au mali au rasilimali zingine, zinazoweza kuchangia kwenye shughuli yoyote isiyoruhusiwa. (2) Kwenye taratibu za hatia chini ya kanuni hii, si lazima kiongozi wa mashtaka athibitishe kuwa anayeshutumiwa alikuwa anajua au alikuwa na sababu ya kujua kuwa ufikishaji wa huduma za fedha, au uhamishaji au mali au rasilimali za fedha, au mali au rasi limali zingine, zinaweza kuchangia kwenye shughuli isiyoruhusiwa. […] (4) Kwenye kanuni hii, “shughuli isiyoruhusiw a” inamaanisha (a) miradi au shughuli zozote zinazohusu nyuklia, makombora ya mbali, au silaha zozote zingine za

Enrico Carisch www.comcapint.com Loraine Rickard-Martin

Simu: (610) 390 9541 110 West 94 Street 2-D Simu: (917) 715 2142

Rico.carisch@comcapint.com New York, NY 10025 loraine.rickard-martin@comcapint.com

ufikishaji wa huduma za fedha zinazochangia kwenye shughuli zisizoruhusiwa. Hii ili maanisha kuwa mchango wa fedha kwenye uhamishaji wa bidhaa yoyote ya uuzaji n je iliyoorodheshwa ukawa hauruhusiwi na sheria ya nchi, *yaani,* ikiwemo kuchangia f edha kwenye uhamishaji wa silaha za kawaida.[40]

Licha ya azimio la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa la 1540 (2004) na mwito w ake kwa Nchi Wanachama kuharamisha shughuli za kufadhili usambazaji, nchi nying i hazitekelezi vikwazo vyote vya fedha vinavyohusu Korea Kaskazini kwenye sheria z ao husika za nchi.[41] Hii inasababisha hali ambapo mashirika ya Korea Kaskazini yana weza kuendelea kufanya shughuli bila wasiwasi kwenye mamlaka nyingi.[42] Kwa hivy o, utekelezaji kamili wa maazimio ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa utasaid ia ufunguliaji mashtaka kwenye kesi kama vile Chinpo.

3.2 Shughuli zinazopitia watu binafsi au mashirika yaliyoorodheshwa

Usafirishaji ulipotokea, OMM ilikuwa haijaorodheshwa kwenye orodha ya vikwazo vy a Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa. Ilichukua zaidi ya mwaka mmoja baada ya

---

maangamizi makubwa za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Korea; au (b) shughuli yoyote inayochukuliwa kuwa ni hatia kwenye paragrafu ya (1) au kanuni za 5, 5A, 6, 7, 8, 8A, 8B(1), 8C, 8D, 8E(1), 9, 9A, 10, 11 au 12A". Sheria z a Singapoo Mtandaoni, "Umoja wa Mataifa (Vikwazo - Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Korea) - Kanuni za 201 0," S 570/2010, https://sso.agc.gov.sg/SL/UNA2001-S570-2010?DocDate=20181213&ValidDate=20181214 (ilifikiwa mnamo 26 Aprili 2019).

[40] Ibid.; Sheria za Singapoo Mtandaoni, "Kifungu cha Saba: Uingizaji Nchini Na Uuzaji Nje Usioruhusiwa Kwa (Ikiwe mo Bidhaa Zilizosafirishwa Kimpito Na Bidhaa Zilizoko Njiani Zilizokuwa Zinatoka Au Zinaelekea Kwenye) Nchi au Ar dhi," *Kanuni ya Uingizaji Nchini na Kanuni za Uuzaji Nje (Cap. 272A, Rg 1),* https://sso.agc.gov.sg/SL/RIEA1995-RG 1?DocDate=20190208&ProvIds=Sc7-&ViewType=Within&Phrase=weapons&WiAl=1 (ilifikiwa mnamo 28 Aprili 2019).

[41] Jonathan Brewer, "Ufadhili wa Usambazaji wa Silaha za Nyuklia na Silaha Zingine za Maangamizi Makubwa," *Kitu o cha Usalama Mpya wa Marekani,* (Januari 2018): 13.

[42] S/2016/157; Brewer, "Ufadhili wa Usambazaji wa Silaha za Nyuklia na Silaha Zingine za Maangamizi Makubwa".

Enrico Carisch www.comcapint.com Loraine Rickard-Martin

Simu: (610) 390 9541 110 West 94 Street 2-D Simu: (917) 715 2142

Rico.carisch@comcapint.com New York, NY 10025 loraine.rickard-martin@comcapi nt.com

mzigo kukamatwa ndipo OMM ikaongezwa kwenye Orodha Jumuishi ya Watu Binafsi na Mashirika Yaliyowekewa Vikwazo na Umoja wa Mataifa.[43] Hata hivyo, Chinpo haija wahi kuorodheshwa.[44] Mbali na haya, licha ya kuorodheshwa, OMM iliendelea kufany a shughuli kwa miaka kadhaa kupitia mikakati ijulikanayo ya ukiukaji.[45]

Hii inaonyesha vikomo vya kupinga usambazaji kupitia mbinu ya ukaguzi unaotege mea orodha.[46] FATF inadokeza kuwa ingawa "ukaguzi wa majina na anwani dhidi ya orodha iliyojumlishwa ya watu binafsi na mashirika yaliyoorodheshwa [⋯] unahitaji ka ili kuhakikisha utiifu wa vipengee fulani vya vikwazo vya fedha vinavyolengwa [⋯] ukaguzi hautotosha kivyake, kwa ajili vikwazo vya fedha vinavyolengwa pia vinahusi sha watu/mashirika yanayofanya shughuli kwa niaba ya au kwa kufuata maagizo ya watu/mashirika yaliyoorodheshwa" .[47] Hii ndiyo ilikuwa hali pale Chinpo ilipokuwa *i nafanya shughuli kwa niaba ya* OMM, bila Chinpo yenyewe kuorodheshwa. Ingawa u kaguzi wa mashirika au watu binafsi wanaofanya shughuli kwa niaba ya watu binafsi au mashirika yaliyoorodheshwa unapendekezwa, bado unabakia kuwa changamoto, kwa sababu si rahisi majina mtawalia yatokee kwenye miamala ya fedha.[48]

---

[43] Erol na Spector, "Chinpo Shipping," 46.

[44] Ibid., 46, 47.

[45] S/2016/157, paragrafu ya 136.

[46] Dall et al. "Kupinga Ufadhili wa Usambazaji," 10.

[47] FATF, *Mwongozo wa Kupinga Ufadhili wa Usambazaji – Utekelezaji wa Masharti ya Fedha ya Maazimio ya Baraz a la Usalama la Umoja wa Mataifa la Kupinga Usambazaji wa Silaha za Maangamizi Makubwa,* (Paris: FATF, 2018), http://www.fatf-gafi.org/publications/fatfrecommendations/documents/guidance-counter-proliferation-financing.html (ilif ikiwa mnamo 26 Aprili 2019), paragrafu ya 19. Vikwazo vye fedha vinavyolengwa pia vitawekewa wale wanaofanya s hughuli kwa niaba ya watu walioorodheshwa, na wale wanaomilikiwa na kudhibitiwa na wao, na wale wanaowasaidia kukwepa vikwazo. FATF, *Mwongozo wa Kupinga Ufadhili wa Usambazaji,* paragrafu ya 27.

[48] Dall et al. "Kupinga Ufadhili wa Usambazaji," 11.

Enrico Carisch www.comcapint.com Loraine Rickard-Martin

Simu: (610) 390 9541 110 West 94 Street 2-D Simu: (917) 715 2142

Rico.carisch@comcapint.com New York, NY 10025 loraine.rickard-martin@comcapint.com

3.3 Utiifu unaotegemea shughuli

Kwa ziada, pendekezo la FATF la kukagua majina ya watu binafsi na mashirika halita tui kikamilifu tatizo linalohusishwa na mbinu za ukaguzi zinazotegemea orodha. Kih alisi, ukaguzi unaotegemea orodha unabakia kuwa hauna ufanisi ikiwa watu binafsi ambao hawajaorodheshwa kwenye vikwazo vya Umoja wa Mataifa wanahusishwa k wenye shughuli za ufadhili wa usambazaji.[49] Hata kwenye kugundua watu binafsi, m binu za ukaguzi zinazohusishwa na taasisi za fedha zina kasoro zao za kimsingi: Prog ramu iliyofanywa otomatiki ambayo mara nyingi inatumiwa kukagua wahusika wa muamala dhidi ya orodha za Vikwazo vya Umoja wa Mataifa inarudisha idadi kubwa sana ya matokeo bandia kwa ajili ya makosa ya kuandika na kufanana kwa majina.[50]

Licha ya haya, Pendekezo la FATF linalohusu ufadhili wa usambazaji linabakia kuwa l inaangazia kwa karibu sana haja ya kutekeleza vikwazo vya fedha vinavyolengwa.[51] V ikwazo vya fedha vinavyolengwa pia vinarejelewa kama ‘vikwazo vinavyotegemea orodha’ kwa ajili vinalazimu ukwamishaji fedha au mali na kuwawekea vizuizi vingi

[49] Rachel A. Weise, Gretchen Hund na Geoffrey Carr, “Vidhibiti vya uuzaji nje na kupinga ufadhili wa usambazaji: pan de mbili za shughuli sawia iliyo haramu ya Silaha za Maangamizi Makubwa,” *Tathmini ya Kupinga Usambazaji ya* 25, namb. ya 1-2 (2018): 137, https://doi.org/10.1080/10736700.2018.1473107 (ilifikiwa mnamo 26 Aprili 2019).

[50] Togzhan Kassenova, “Changamoto Kwenye Utekelezaji wa Vidhibiti vya Ufadhili wa Usambazaji: Jinsi Vidhibiti vya Uuzaji Nje Vinavyoweza Kusaidia,” *ECR Ulimwenguni: Jarida la 69 la Vidhibiti vya Uuzaji Nje na Vikwazo* (Mei 2018), https://carnegieendowment.org/2018/05/30/challenges-with-implementing-proliferation-financing-controls-how-export-controls-can-help-pub-76476 (ilifikiwa mnamo 26 Aprili 2019); Weise et al., “Vidhibiti vya Uuzaji Nje na Kupinga Ufad hili wa Usambazaji,” 137.

[51] Pendekezo la 7 la FATF linaziambia nchi “zitekeleze vikwazo vy fedha vinvyolengwa ili kutii maazimio ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kuhusu uzuiaji, usitishaji, na ukatizaji wa usambazaji wa silaha za maangamizi makub wa na ufadhili wake”. FATF, *Viwango vya Kimataifa vya Kupinga Ulanguzi wa Pesa na Ufadhili wa Ugaidi na Usamb azaji: Mapendekezo ya FATF*, (Paris, FATF: 2012-2018), www.fatrf-gafi.org/recommendations.html (ilifikiwa mnamo 2 6 Aprili 2019), Pendekezo la 7.

Enrico Carisch www.comcapint.com Loraine Rickard-Martin

Simu: (610) 390 9541 110 West 94 Street 2-D Simu: (917) 715 2142

Rico.carisch@comcapint.com New York, NY 10025 loraine.rickard-martin@comcapi nt.com

ne *watu binafsi na mashirika yaliyoorodheshwa*.[52] Mfano wa Chinpo umeonyesha ku wa uwezo wa Korea Kaskazini kufanya shughuli kupitia kampuni zifichazo na watu w a mpito wasioorodheshwa hawatozuiwa kwa kudumusha makini tu kwenye vikwazo vya fedha vinavyolengwa.

Taasisi za fedha zenye hamu ya kuepuka ufadhili wa usambazaji zinafaa pia kuangaz ia utekelezaji wa makatazo ya huduma za fedha zinazochangia *shughuli zisizoruhusi wa*.[53] Makatazo ya fedha yanayotegemea shughuli yana mkono mrefu kuliko vikwazo vinavyotegemea orodha. Yanalenga kuzuia miamala hata ikiwa hakuna shirika au mt u binafsi aliyewekewa vikwazo anayehusika moja kwa moja kwenye muamala.[54] Kwa hivyo, vidhibiti vinavyotegemea shughuli ni bora kwenye kuzuia mifano kama vile Ch inpo.

Kutekeleza ukaguzi wa kutegemea shughuli ni changamoto kwa ajili ni ngumu zaidi na kunatumia muda mwingi zaidi, yaani, kunaleta gharama zaidi kwa taasisi za fedh a, kuliko mbinu za ukaguzi zinazotegemea orodha ambazo zimefanywa otomatiki.[55] I li kuhusisha mbinu za ukaguzi zinazotegemea shughuli, taasisi za fedha zinahitaji kuj

---

[52] Brewer, "Ufadhili wa Usambazaji wa Nyuklia na Silaha Zingine za Maangamizi Makubwa," 4; Eda Erol na Leonard S. Spector, "Hatua Zijazo Zinazohitajika ili Kuimarisha Hatua za Kupinga Ufadhili wa Usambazaji," *Kituo cha Utafiti w a Kupinga Usambazaji cha James Martin Ripoti ya Kanuni ya* 35 (Disemba 2017): 31; Weise et al., "Vidhibiti vya uuza ji nje na kupinga ufadhili wa usambazaji," 134.

[53] Weise et al., "Vidhibiti vya uuzaji nje na kupinga ufadhili wa usambazaji," 134.

[54] Ibid.

[55] Ibid.

Enrico Carisch www.comcapint.com Loraine Rickard-Martin

Simu: (610) 390 9541 110 West 94 Street 2-D Simu: (917) 715 2142

Rico.carisch@comcapint.com New York, NY 10025 loraine.rickard-martin@comcapi nt.com

ua jinsi ya kutambua shughuli za usambazaji.[56] Lakini, taasisi za fedha hazina uwezo wa kung'amua ni shughuli zipi ambazo zinahusu usambazaji.[57]

Ili kuufanya ukaguzi unaotegemea shughuli ufanye kazi, uwezo wa taasisi za fedha k utambua shughuli za usambazaji ni lazima ukuzwe. Hii inaweza kufanywa kwa kutoa mwongozo kuhusu uainishaji wa usambazaji.[58] Imependekezwa kuwa taasisi za fedh a zinafaa kuwekeza kwenye matendo ya kudhibiti hatari yanayojumuisha ishara za h atari za usambazaji, na kwenye kuelimisha maafisa wao wa utiifu.[59] Kwa ziada, taasis i za fedha zinafaa kusombeza michakato yao ya ukaguzi yaliyofanywa otomatiki ili y achukue hatua zaidi kuliko zile zinazochukuliwa na ukaguzi unaotegemea orodha.[60] Ushirikiano baina ya taasisi za fedha, ujasusi wa fedha, wadhibiti fedha, na pia maml aka za ushuru na za kudhibiti uuzaji nje unawezo kuleta pamoja utaalamu unaohitaji ka ili kutathmini hatari za kuchangia kwenye shughuli za usambazaji.[61] Taasisi za fed ha hazihitaji tu kuulizia kama miamala inahusisha mashirika yaliyoorodheshwa, laki ni pia ikiwa kama matumizi ya mwisho na lengo la muamala ni halali.[62]

3.4 Haja ya mifumo ya utiifu inayotegemea hatari

[56] Ibid., 137.

[57] Kassenova, “Changamoto Kwenye Utekelezaji wa Vidhibiti vya Ufadhili wa Usambazaji”; Brewer, “Uchunguzi wa U ainishaji” 9.

[58] Ibid.; Weise et al., “Vidhibiti vya uuzaji nje na kupinga ufadhili wa usambazaji,” 138.

[59] Kassenova, “Changamoto Kwenye Utekelezaji wa Vidhibiti vya Ufadhili wa Usambazaji”.

[60] Ibid.; Weise et al., “Vidhibiti vya uuzaji nje na kupinga ufadhili wa usambazaji,” 138.

[61] Kassenova, “Changamoto Kwenye Utekelezaji wa Vidhibiti vya Ufadhili wa Usambazaji”; cf. Erol na Spector, “Hatu a Zijazo Zinazohitajika ili Kuimarisha Hatua za Kupinga Ufadhili wa Usambazaji”.

[62] Kassenova, “Changamoto Kwenye Utekelezaji wa Vidhibiti vya Ufadhili wa Usambazaji”

Enrico Carisch www.comcapint.com Loraine Rickard-Martin

Simu: (610) 390 9541 110 West 94 Street 2-D Simu: (917) 715 2142

Rico.carisch@comcapint.com New York, NY 10025 loraine.rickard-martin@comcapint.com

Taasisi ya fedha iliyohusishwa ilishindwa kutii uangalifu unaoeleweka ambao ulikuw a unahitajika kuhusiana na miamala ya Chinpo. Uchunguzi wa kesi hii ulifichua kuwa miamala ya kiasi kikubwa ilitekelezwa bila Benki ya Uchina (BoC) kuonyesha wasiwa si wowote. "Tahadhari nyekundu" zilikuwa zinafaa kuripotiwa na BoC: Ghafla, Chi npo iliondoa majina ya vyombo vya usafiri kwenye miamala;[63] utoaji pesa wa kiasi ki kubwa cha hadi $500,000 kutoka akaunti ya Chinpo uliofanywa na mwanadiplomasi a wa Korea Kaskazini;[64] na Chinpo kuwa na uhusiano wa karibu na Korea Kaskazini. K wa kuzingatia tahadhari hizi nyekundu na biashara ya usafirishaji ya kampuni hii, ilik uwa inafaa kushughulikiwa kwenye kategoria ya hatari kubwa.[65] Kwa kushangaza, B oC ilishindwa kuulizia kuhusu mapato ya Chinpo kwenye matukio yote isipokuwa m oja. Uuliziaji pekee uliotokea ulihusu *Chong Chon Gang* kusafiri hadi Kuba, ambayo ilizindua arifa kuhusu vikwazo vya Umoja wa Mataifa vilivyowekewa Kuba. Sababu z a uuliziaji huu kwa hivyo hazikuwa, kama zilivyofaa kuwa, wasiwasi kuhusu vikwazo vilivyowekewa Korea Kaskazini.[66]

Ili kutatua kushindwa kwa utiifu, taasisi za fedha zinafaa kuhusisha uangalifu unaoel eweka ambao umekuzwa kwenye miamala yenye hatari zaidi ya kuchangia usambaz aji wa nyuklia. Ili kutambua hatari, mbinu inayotegemea hatari ya kupinga ufadhili w a usambazaji zinafaa kuhusishwa. Taasisi za fedha zinaweza kulazimishwa zitathmin i, zikague na zifuatilie hatari zao za kuchangia kwenye ufadhili wa usambazaji na zich ukue hatua ili kupunguza hatari hizo.[67] Sababu za hatari zinaweza kutambuliwa kupi

[63] Dall et al. "Kupinga Ufadhili wa Usambazaji," 14.

[64] Ibid.

[65] Ibid.

[66] Brewer, "Utafiti wa Uainishaji" 54.

[67] Brewer, "Ufadhili wa Silaha za Nyuklia na Silaha ZIngine za Maangamizi Makubwa," 14.

Enrico Carisch www.comcapint.com Loraine Rickard-Martin

Simu: (610) 390 9541 110 West 94 Street 2-D Simu: (917) 715 2142

Rico.carisch@comcapint.com New York, NY 10025 loraine.rickard-martin@comcapint.com

tia tathmini za wateja, nchi au maeneo ya kijiografia, bidhaa, huduma au vituo vya bi ashara vinavyojihusisha na.[68]

Pendekezo la kwanza la FATF linahitaji nchi zihusishe mbinu inayotegemea hatari na zichukue hatua ili kuzuia na kupunguza hatari za *ulanguzi wa pesa, na ufadhili wa ug aidi*.[69] Licha ya haya, pendekezo hazipanui mahitaji haya yahusishe kupinga ufadhili wa usambazaji. Kwa ajili mbinu ya kutegemea hatari pia inahusika kisawia kwenye k upinga ufadhili wa usambazaji, huu ni udhaifu madhubuti wa Mapendekezo ya FATF [70]

Haswa, pendekezo la 1 linatoa mwito nchi zihakikishe kuwa mfumo wao wa kupinga ulanguzi wa pesa na kupinga ufadhili wa ugaidi unazishughulikia vilivyo na kuzipung uza hatari kubwa.[71] Nchi zinafaa kuzilazimu taasisi zao za fedha zihusishe hatua ziliz okuzwa za kupunguza hatari ikiwa hatari kubwa zimetambuliwa.[72] Haja hii – ambayo FATF haipendekezi kwa uwazi ili kupinga ufadhili wa usambazaji – ingekuwa inahitaj ika ili kushughulikia miamala ya Chinpo.

---

[68] Ibid., 16.

[69] FATF, *Mapendekezo ya FATF*, Pendekezo la 1.

[70] Ukweli ni kuwa mawili kati ya Mapendekezo 40 ya FATF yanahusisha wazi ufadhili wa usambazaji umetambuliwa k ama udhaifu madhubuti wa mfumo wa FATF. Mapendekezo mengi mengine huwa pia yanahusisha CPF. Brewer, “Uf adhili wa Silaha za Nyuklia na Silaha ZIngine za Maangamizi Makubwa,” 14.

[71] FATF, *Mapendekezo ya FATF*, 9, 29.

[72] Ibid., 29, 30.

Enrico Carisch www.comcapint.com Loraine Rickard-Martin

Simu: (610) 390 9541 110 West 94 Street 2-D Simu: (917) 715 2142

Rico.carisch@comcapint.com New York, NY 10025 loraine.rickard-martin@comcapint.com

Kwa hivyo, pendekezo la 1 linafaa kupanuliwa lijumuishe kupinga ufadhili wa usamb azaji. Zaidi ya haya, mbinu inayotegemea hatari haifai kuhusishwa kwenye kupinga ufadhili wa usambazaji tu, bali pia kwenye kupinga ufadhili wa biashara ya silaha za kawaida na Korea Kaskazini. Kesi ya Chinpo inaashiria kuwa uhusishaji mpana zaidi wa mbinu inayotegemea hatari inayotumiwa na taasisi za fedha unahitajika ili kuzui a kuenda kinyume na vikwazo vya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa.

	Beatrice Müller ana shahada ya kwanza kwenye Sayansi ya Kisiasa na sh ahada ya uzamili kwenye mafunzo ya Mashariki ya Kati kutoka Chuo Kik uu cha Geneva. Kwa sasa anafanya kazi kwenye nyanja ya udhibiti wa si laha, upingaji usambazaji na upokonyaji silaha, huku pia alipokuwa anaf anya kazi kama mhariri mwenza wa masuala ya mambo ya nje kwenye kituo cha utafiti cha Uswizi kiitwacho *foraus*. Hapo awali, Bi. Müller alik uwa mkufunzi na kufanya kazi kwenye NGO ya haki za binadamu na Mu ungano wa Mabunge.

Enrico Carisch www.comcapint.com Loraine Rickard-Martin

Simu: (610) 390 9541 110 West 94 Street 2-D Simu: (917) 715 2142

Rico.carisch@comcapint.com New York, NY 10025 loraine.rickard-martin@comcapint.com